



SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR
WIZARA YA HABARI UTALII NA MAMBO YA KALE

Tel: 0255 24 2237325/0255 24 223 7313
Fax: 0255 24 2237314
Website: www.dis.go.tz
Email : maelezozanzibar@gmail.com

Idara ya Habari Maelezo
P.O. Box 2754
Zanzibar

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Katika Kujikinga na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa Corona na kuepuka mikusanyiko , Kuanzia leo Aprili 13 mwaka 2020 Mikutano ya Waandishi wa Habari na shughuli nyengine zitakazowafanya waandishi wa habari kukusanyika zinasitishwa.

Hivyo, basi taarifa za Waziri wa Afya Zanzibar kuhusiana na Virusi vya ugonjwa wa Corona zitatolewa kwa njia ya 'Press Releases', kurusha moja kwa moja kupitia Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) au kurekodiwa na kusambaza taarifa hiyo kwa vyombo vya habari na umma kwa ujumla.

Taasisi zote zenye shughuli zitakazowajumuisha waandishi wa habari tunawaomba kutumia njia tulizozieleza na kujiepusha kwa namna yoyote ile kuwaita waandishi wa habari katika shughuli zao.

Wahariri na waandishi wa habari tunawasisitiza kufuata maelekezo ya wataalamu wa afya na Serikali kwa ujumla kwa kuepuka mikusanyiko

Dkt Juma Mohammed Salum

Mkurugenzi

Idara ya Habari (MAELEZO) Zanzibar

13 Aprili, 2020